

Kukosa uvumilivu wa kidini

Habari kwa wazazi, walezi na wanafunzi

Ahadi yetu

Idara hutambua, huthamini na huheshimu tofauti za kilugha, kidini na kiroho za wanafunzi, familia zao na jumuiya ya shule. Tumejitolea kukomesha aina zote za ubaguzi katika shule za serikali za NSW.

Je, kukosa uvumilivu wa kidini ni nini?

Kukosa uvumilivu wa kidini huko wakati mtu ni mkatili, hana haki au anawatendea wengine kwa njia tofauti kwa sababu ya dini yao, imani, au hali ya kiroho.

Jinsi gani wanafunzi wanaweza kutoa taarifa za kukosa uvumilivu wa kidini

Wanafunzi ambao wanapitia kukosa uvumilivu wanapaswa kutoa ripoti juu yake kwa mwalimu au mfanyakazi wa shule. Pia wanafunzi wanaweza kupiga simu au kutuma barua pepe shuleni kwa kutumia maelezo ya mawasiliano kwenye tovuti ya shule zao.

Pengine kukosa uvumilivu kuna kipengele cha rangi. Ripoti za ubaguzi wa rangi zinaweza kutolewa kwa mfanyakazi yeyote wa shule au kwa [Afisa wa Mawasiliano ya Ubaguzi wa Rangi](#) (Anti-Racism Contact Officer) shuleni. Kupata habari zaidi angalia kurasa ya [Ripoti za ubaguzi wa rangi](#) (Reports of racism) na ya [Sera ya kupinga ubaguzi wa rangi](#) (Anti-racism policy).

Je, usaidizi gani unapatikana kwa wanafunzi?

Kupitia au kushuhudia kukosa uvumilivu wa kidini kunaweza kuwa na athari mbaya kwa wanafunzi. Habari na huduma kwa wanafunzi zinapatikana kwenye tovuti zifuatazo:

- [Usaidizi wa afya ya akili kwa wanafunzi](#) (Mental health support for students)
- [Kurasa za kupinga uonevu kwa wanafunzi](#) (Student anti-bullying pages)

Jinsi gani wazazi, walezi na wanajamii wanaweza kutoa ripoti za kukosa uvumilivu wa kidini

Wazazi, walezi na wanajamii wanaweza kutoa ripoti ya kukosa uvumilivu wa kidini kwa ajili yao wenyewe au kwa ajili ya mwanafunzi kwa ruhusa yake.

Ripoti hiyo inapaswa kutolewa kwa shule ambapo tukio la kutovumiliana kwa kidini lilitokea. Wazazi na walezi wanaweza kutoa ripoti kwa mtu, kwa barua pepe au simu kwa kutumia maelezo ya mawasiliano kwenye tovuti ya shule.

Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia wakati unapowasiliana na shule, piga simu kwa Huduma ya mkalimani wa simu kwenye 131 450 na umwambie mpigaji simu lugha unayohitaji na pia nambari ya simu unayotaka kupiga simu. Hutatozwa kwa huduma hii.

Usaidizi gani unapatikana kwa wazazi?

Habari na usaidizi kwa wazazi hupatikana kwenye tovuti zifuatazo:

- [Usaidizi wa afya na ustawi wa akili](#) (Mental health and wellbeing support)
- [Usaidizi gani unapatikana kwa wazazi?](#) (What support is available to parents?)

Hatua zaidi

Kupata usaidizi zaidi au ikiwa unaamini kukosa uvumilivu kunatokea kwenye mfumo, tumia Simu ya Usaidizi ya Kukosa Uvumilivu kwa kupiga simu kwa 1300 679 332 na umjulishe mpigaji simu kuwa simu ni kuhusu kukosa uvumilivu. Tumia Huduma ya mkalimani wa simu ikihitajika. Simu ya Usaidizi inaweza:

- kutoa habari kuhusu sera na taratibu zinazohusiana
- kuelekeza ripoti kwa maeneo husika
- kupendekeza huduma zinazofaa za usaidizi
- kuamua utatuzi wenye haki kwa ripoti.

Kutoa malalamiko

Wanafunzi, wazazi au walezi wanaweza kutoa malalamiko kwa kufuata hatua katika [mwongozo wa marejeleo wa haraka](#) (quick reference guide for making a complaint) uliotafsiriwa. Jifunze zaidi kuhusu malalamiko kwenye ukurasa uliotafsiriwa wa [watu wasaidizi na watetezi](#) (support persons and advocates).

Sera za idara zinazohusiana

- [Sera ya kupinga ubaguzi wa rangi](#) (Anti-racism policy)
- [Sera ya elimu ya tamaduni nyingi](#) (Multicultural education policy)
- [Sera ya tabia ya mwanafunzi](#) (Student behaviour policy)